

Salim Ahmed Salim

## OFISI YA DR. SALIM AHMED SALIM

Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania  
Katibu Mkuu Mstaafu wa Jumuiya ya Muungano wa Nchi za Afrika (OAU)

23 Januari, 2024

### TOVUTI YA HIFADHI YA NYARAKA ZA DKT. SALIM AHMED SALIM YATOA MATOLEO MAPYA YA NYARAKA KUADHIMISHA MIAKA 82 YA KUZALIWA DKT. SALIM

**Dar es Salaam:** Dkt. Salim Ahmed Salim, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na, Katibu Mkuu Mstaafu wa Jumuiya ya Muungano wa Nchi za Afrika (kwa sasa Umoja wa Afrika), anatembea miaka 82 leo na kama sehemu ya kusherehekea umri wake mpya, Tovuti ya Hifadhi ya Nyaraka zake ([www.salimahmedsalim.com](http://www.salimahmedsalim.com)) imetoa matoleo mapya ya nyaraka yanayojumuisha matukio mbalimbali ya kihistoria barani Afrika na ulimwenguni.

Matoleo mapya, yanayojumuisha nakala za mawasiliano ya kimaandishi za Dkt. Salim, ni pamoja na:

- Israeli-Palestina:** Mkutano baina ya Dkt. Salim na Yasser Arafat – aliyekuwa Kiongozi Mkuu wa Chama cha Ukombozi wa Palestina (PLO) – uliofanyika tarehe 11 Machi, 1990 na kuzungumzia hoja na wasiwasi wa PLO juu ya upanuzi wa Israeli;
- Mkutano wa Geneva kuhusu Rhodesia:** Sehemu ya kwanza ya nakala za mawasiliano ya kimaandishi juu ya Mkutano wa Geneva uliozungumzia Rhodesia (kwa sasa Zimbabwe), ambao ulikuwa ni jitahada za Uingereza za kufika mwafaka wa kupata sera ya uhuru nchini Rhodesia;
- Historia ya Marekani:** Barua ya Hayati Coretta Scott King, mwanaharakati wa haki za kiraia na mke wa Hayati Rev. Martin Luther King (Jr.), kwenda kwa Dkt. Salim, mnamo mwaka 1979;
- Mkutano baina ya Tanzania na Libya:** Nakala za mawasiliano ya kimaandishi za Dkt. Salim katika mkutano baina yake na Rais wa Libya, Hayati Muammar Ghadafi, tarehe 13 Machi, 1990.

Akizungumza kwa niaba ya Familia ya Dkt. Salim na Tovuti ya Hifadhi ya Nyaraka za Dkt. Salim, Ahmed Salim (ambaye pia ni Mtoto wa Dkt. Salim), alisema:

*“Matoleo mapya ni sehemu ya zoezi la kuboresha maudhui ya tovuti, litakalofanyika kila baada ya miezi 3 – 4. Tumaini letu ni kwamba nyaraka hizi, ambazo ni nyongeza ya zile zilizomo kwenye tovuti, zitaibua mijadala juu ya siasa za Kiafrika na kimataifa, na umuhimu wa uhusiano na nchi mbalimbali katika nyakati zisizotabirika.”*

Tovuti ya Dkt. Salim, ambayo ni ya kwanza ya aina yake nchini Tanzania, ni kavazi la siasa za kimataifa na jukwaa la kipekee linaloonyesha nafasi muhimu iliyochezwa na viongozi na nchi za Kiafrika katika jitihada za kuleta amani na utulivu duniani. Inaishamirisha Tovuti ya Hifadhi ya Nyaraka za Rais Nelson Mandela, ambalo ni kavazi lingine la kidigitali barani Afrika linaloweza kufikiwa na mtu yeyote.

**\*\*MWISHO\*\***